Taarifa kwa vyombo vya habari | 30 Agosti 2017

Wananchi wengi wanatumia vituo vya afya vya serikali na husubiri chini ya saa moja kumuona daktari

Wakati huo huo, wananchi 7 kati ya 10 wanasema changamoto ipo katika upatikaji wa dawa na vifaa tiba

30 Agosti 2017, Dar es Salaam: Wananchi wanapopata majeraha ama kuugua, 6 kati ya 10 (61%) huenda katika kituo cha afya cha serikali. Kiwango hiki kimeongezeka kutoka 45% mwaka 2014 na kubaki hivyo hivyo tangu mwaka 2016. Kwa kiasi kikubwa hii imesababishwa na kupungua kwa watu wanaojitibu wenyewe kwa kwenda kwenye maduka ya dawa (9%), maduka ya kawaida kupata dawa (7%), wasiofanya chochote (1%) au wanaotafuta aina nyingine za matibabu (5%). Takwimu zilizokusanywa toka mwaka 2014 zinaonesha kupungua kwa matumizi ya njia hizo. Idadi ya wananchi wanaotumia vituo binafsi, vya kanisa ama vya mashirika yasiyo ya kiserikali haijabadilika katika kipindi hiki (16% mwaka 2017).

Pamoja na ongezeko la idadi ya wagonjwa, utaratibu wa wananchi kusubiri kwa saa moja ama chini ya hapo ili kumuona daktari haujabadilika toka mwaka 2014. Wananchi 7 kati ya 10 (70%) walisubiri kwa saa moja ama chini ya hapo mwaka 2014 ukilinganisha na wananchi 3 kati ya 4 (76%) mwaka 2017. Hata hivyo, wagonjwa husubiri kwa saa moja ama chini ya hapo katika vituo binafsi, vya kanisa ama vya mashirika yasiyo ya kiserikali (88% walisubiri kwa muda huu) ukilinganisha na vituo vya serikali (74% walisubiri kwa saa moja ama chini ya hapo).

Matokeo haya yametolewa na Twaweza katika utafiti wake uitwao *Afya kwanza! Wasemavyo wananchi kuhusu huduma za afya*. Muhtasari unatokana na takwimu za *Sauti za Wananchi,* utafiti wa kwanza barani Afrika, wenye uwakilishi wa kitaifa unaotumia simu za mikononi. Matokeo haya yanatokana na takwimu zilizokusanywa kutoka kwa wahojiwa 1,801 kutoka maeneo mbalimbali ya Tanzania Bara (Zanzibar haihusiki kwenye utafiti huu) mwezi Mei 2017.

Wananchi wengi wanaridhishwa na usafi katika vituo vya afya. Wananchi wanaosema hili bado ni tatizo wamepungua kutoka 29% mwaka 2015 hadi 9% mwaka 2017 na 42% walilalamikia kiwango cha kuheshimiwa na kujaliwa na wahudumu mwaka 2015 ukilinganisha na 26% mwaka 2017.

Pamoja na maboresho haya, wananchi wanaendelea kukumbana na changamoto kubwa wakati wakipata huduma za afya. Wananchi watatu kati ya kumi ambao walimsindikiza mtu hospitali mwaka uliopita (29%) walikuta wagonjwa wawili ama zaidi wakichangia vitanda na magodoro. Kuna mabadiliko kutoka mwaka 2016 ambapo karibu wananchi 4 kati ya 10 (36%) walishuhudia wagonjwa wakichangia vitanda/magodoro.

Inatia mashaka zaidi linapokuja suala la upatikanaji wa dawa na vifaa tiba. Toka mwaka 2015, kumekuwa na ongezeko la wananchi waliokutana na upungufu wa dawa/vifaa tiba mara ya mwisho walipoenda katika kituo cha afya cha serikali. Vilevile, kuna ongezeko la wananchi ambao wanalalamikia muda wa kusubiri, kutoka 53% mwaka 2015 hadi 63% mwaka 2017.

Linapokuja suala la upatikanaji wa madaktari na gharama za huduma, idadi ya wananchi waliokuwa wanalalamikia masuala haya walipungua kati ya mwaka 2015 na 2016, lakini idadi imeongezeka tena mwaka 2017.

- Ukosefu wa madaktari lilikuwa ni tatizo kwa 43% mwaka 2015, likashuka mpaka 18% mwaka 2016 na kupanda mpaka 29% mwaka 2017.
- Gharama za huduma ilikuwa ni tatizo kwa wananchi 34% mwaka 2015, 19% mwaka 2016 na 28% mwaka 2017.

Twaweza pia iliwauliza wananchi iwapo sera ya serikali inatekelezwa kwa uzoefu wao,

- Watoto wenye umri chini ya miaka mitano, wazee na wajawazito wanapaswa kupata matibabu bure katika vituo vya afya vya serikali. Tangu mwaka 2016 kumekuwa na ongezeko dogo la idadi ya watu kutoka kwenye makundi hayo wanaopata huduma za matibabu bila malipo lakini wengi wao wanalazimishwa kulipa. **Miongoni mwa wananchi waliowasindikiza watoto, wajawazito na wazee, 35% walilazimika kulipia matibabu ya mtoto, 28% ya wajawazito na 37% ya wazee.**
- Pamoja na kauli za serikali na wananchi 84% kuwa waathirika wa ajali, ugomvi au majeraha watibiwe kabla ya kupata kibali kutoka polisi, wananchi **6 kati ya 10 waliowasindikiza waathirika hao ili kupata matibabu walitakiwa kupata kibali cha polisi kabla ya kupata matibabu.**
- Bima, hususani kupitia Mfuko wa Afya ya Jamii ulioboreshwa, ni mkakati mkubwa wa serikali wa kupanua upatikanaji wa huduma za afya. **Kati ya mwaka 2014 na 2017 idadi ya watu wenye bima ya afya imeongezeka kutoka 21% hadi 27%.** Kwa ujumla, 13% ya wananchi wanasema ni wanachama wa Mfuko wa Afya ya Jamii (ulioboreshwa). Kwa kiwango cha ongezeko la sasa, Tanzania huenda ikafikia kiwango cha kimataifa cha wananchi wake kufikiwa na bima ya afya ndani ya miaka 40 ijayo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Twaweza Aidan Eyakuze, anasema: "*Tunaweza kuyafurahia baadhi ya matokeo haya. Wananchi wanatumia zaidi vituo vya afya vya serikali na baadhi ya masuala katika utoaji wa huduma za afya yameboreshwa. Lakini tatizo la dawa na vifaa tiba, sambamba na uchache wa watendaji wa afya, bado ni tatizo kubwa.*"

"Jambo lingine linalotia mashaka," anaendelea "ni namna ambavyo sera ya serikali inapuuzwa na watoa huduma za afya. Kwani pamoja na kauli kali za serikali na kampeni za kuelimisha umma, huduma bure ya afya haitolewi ipasavyo kwa makundi ya wananchi wanaostahili huduma bure. Lazima tuendelee kufuatilia na kukumbushana kuwa utamaduni wa uwajibikaji ni kiungo muhimu sana kwa maendeleo ya sekta yetu ya afya."

---- Tamati----

Kwa taarifa zaidi wasiliana na:
Risha Chande, Mshauri Mwandamizi wa Mawasiliano, Twaweza
Barua pepe: rchande@twaweza.org | **Simu:** (+255) (0) 656 657 559

Maelezo kwa Wahariri

- Muhtasari huu na takwimu zake zinapatikana kupitia www.twaweza.org, au www.twaweza.org/sauti
- Twaweza inafanya kazi ya kupima uwezo wa watoto kujifunza, wananchi kuwa na utayari wa kuleta mabadiliko na serikali kuwa wazi na sikivu zaidi katika nchi za Tanzania, Kenya na Uganda. Twaweza ina programu, wafanyakazi na ofisi katika nchi zote tatu, na mfumo unaoheshimika

kimataifa wa kujifunza, ufuatiliaji na tathmini. Programu zetu muhimu ni pamoja na Uwezo, ambayo ni tathmini kubwa ya kila mwaka ya wananchi barani Afrika inayopima viwango vya watoto vya kujifunza kwenye maelfu ya kaya na *Sauti za Wananchi*, utafiti wa kwanza barani Afrika wenye uwakilishi wa kitaifa unaofanyika kwa njia ya simu za mkononi. Pia tunashiriki katika masuala ya umma na sera kupitia ubia wetu na taasisi mbalimbali pamoja na vyombo vya habari. Vile vile Twaweza inashiriki na kuratibu jitihada za kimataifa zinazoshughulikia masuala ya uwazi, uwajibikaji na Ushirikishwaji kama vile mkakati wa kimataifa wa kuendesha shughuli za serikari kwa uwazi (OGP).

- **Tovuti:** www.twaweza.org **Facebook:** Twaweza Tanzania **Twita:** @Twaweza_NiSisi